# Same and Mwanga Environmental Conservation Advisory Organization (SMECAO)

TOLEO LA PILI

JULAI, 2012



SMECAO FUND,

P.O BOX 87,

SAME - KILIMANJARO,

Email: smecao@gmail.com,

smecao@elct.org,

Website: www.smecao.jimdo.com

# TUBADILIKE!

# Safu ya wafanyakazi Same and Mwanga Environmental Conservation Advisory Organization (SMECAO)



**BIBI VENERANDA SACHORE**
Mkurugenzi wa SMECAO



**BIBI LENNA MSUYA**
Mratibu



**SUSAN G. KAGIZE**
Mkuu wa Idara ya Ujasiriamali na Usawa wa Jinsia




**ATHUMANI SUBA**
Fundi Sanifu wa Majiko



**LUKAS JEREMIA**
Dereva



**BENARD W.MKWIZU**
Mkuu wa Idara ya Sheria na Haki za Binadamu



**JANIS HANF**
MFANYAKAZI WA KUJITOLEA WELT WAERTS,
Solivol Project Ujerumani



**ALPHONCE SAMBURA**
Mkuu wa Idara ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabia Nchi



**PAUL PETER NYINDO**
Mkuu wa Idara ya Afya na Ukimwi

# SALAAM TOKA KWA MKURUGENZI WA SMECAO



**Bibi Veneranda A. Sachore**

**Mkurugenzi wa SMECAO**

Wapendwa wasomaji wa Jarida la *TUBADILIKE,* kwa mara nyingine tena napenda kuwakaribisha kusoma toleo la pili la jarida hili baada ya lile la Julai 2011. Kupitia jarida hili wanafunzi na wanajamii kwa ujumla wanapata fursa ya kuelimishana na kuku mbushana juu ya maswala mbalimbali yahusuyo maambukizi ya Virusi vya ukimwi na Ugonjwa wa Ukimwi.

Jarida la TUBADILIKE ni mojawapo ya nyenzo za kuleta ushawishi kwa wanafunzi na jamii kubadili tabia hatarishi zinazopelekea maambukizi ya Virusi vya Ukimwi na kupinga unyanyapaa.

Kwa mwaka 2011/2012, SMECAO Katika harakati za kupambana na ugonjwa wa Ukimwi imeelimisha jamii kupitia mikutano ya hadhara, maonyesho ya picha za video, sanaa za maigizo, ngoma na vichekesho. Vilevile imewajengea uwezo Kamati za kupambana na Ukimwi ngazi ya vijiji, na pia kuendesha mijadala juu ya maambukizi ya Virusi vya Ukimwi na unyanyapaa katika baadhi ya shule za sekondari.

Wapendwa wanaharakati wenzangu, ingawaje takwimu zinaonyesha kuwa kiwango cha maambukizi ya Virusi vya Ukimwi kwa watu wazima kimeshuka toka asilimia 7% - 5.7% kati ya mwaka 2003 - 2008; Takwimu hizi bado hazileti faraja ya kupunguza mapambano kwani pamoja na juhudi ambazo zimefanywa na wadau mbalimbali za kuzuia maambukizi ya VVU kwa zaidi ya miaka 25 bado hali si nzuri kwani kwa mwaka 2009, "Joint United Nations Programme on HIV/AIDS" (UNAIDS) imetoa takwimu na kukadiria kuwa idadi ya watu zaidi ya 130,000 Tanzania wenye umri kati ya miaka 15-49 wanaambukizwa Virusi vya Ukimwi kila mwaka. Kwa mantiki hii bado kuna haja ya kuongeza mapambano kwa kila mmoja wetu katika nafasi yake dhidi ya maambukizi mapya.

Tukumbuke kuwa inakadiriwa asilimia 80% ya maambukizi yote yanasababishwa na ngono isiyosalama. Natoa rai kwa vijana wote kusema "hapana" kwa ngono, kwani takwimu zilizotolewa na "Tanzania HIV/ AIDS Malaria Indicator Survey 2007-2008" (THMIS) inaonyesha kuwa hapa Tanzania asilimia 11% ya vijana ambao wako chini ya umri wa miaka 15 wanajihusisha na ngono.

Karibuni tena wanafunzi wote kusoma na kupata hamasa ya kujikinga na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi kwa kubadili Tabia, mienendo isiyofaa, na fikra potofu zinazopelekea maambukizi ya VVU, lakini pia kuwa chachu kwa jamii nzima katika mapambano dhidi ya VVU.

**MABADILIKO YANA WEZEKANA CHUKUA HATUA**
**PAMOJA TUTASHINDA!**

**"TUBADILIKE"**
**Jarida Toleo la Pili, Julai 2012**

# WANAFUNZI "TUBADILIKE", SUBIRI MAPENZI YANA WAKATI WAKE!!

Kulikuwa na familia moja ya mzee Bryton iliyokuwa ikiishi katika kijiji kimoja wilaya ya Moshi vijijini mkoani Kilimanjaro. Mzee Bryton alikuwa na watoto saba na mke wake aliyekuwa akiitwa Maria. Alikuwa na watoto wa kike watatu na wakiume wanne, mzee Briton alifanikiwa kuwatunza katika maadili mema.

Alikuwa na mtoto wake wa kike aliyeitwa Noela, msichana mzuri mtanashati na mwenye kuvutia mwenye afya nzuri. Wazazi wake walimpenda sana kwasababu alikuwa na heshima na alikuwa akifanya vizuri katika masomo yake.

Noela alipokuwa anasoma kidato cha tatu akaanza kujiunga na makundi mabaya baada ya baba yake kumuhamishia shule nyingine akiwa kidato cha pili. Wazazi wake walimuhamisha shule kutokana na maendeleo yake kutokua mazuri.Noela baada ya kujiingiza kwenye makundi mabaya akaanza kukataa shule ikampelekea kubadilika kitabia akiwa mdogo. Noela akaanza kujiingiza kwenye makundi mabaya, yakiwemo ya kunywa pomb, madawa ya kulevya na ngono, kila aliyemwambia nakupenda hakumkatalia na wengi alishirikiana nao kimwili. Maisha ya Noela yakawa ni ya kutangatanga ingawa bado alikuwa anaenda shule lakini kitendo hicho cha Noela wazazi wake hawakukijua kutokaka na shule aliyopelekwa kuwa mbali na wazazi, na wazazi wake walikuwa bado wanamtegemea kwani Noela peke yake ndo alikuwa na bidii katika masomo.

Noela akapata rafiki aliyeitwa Jonathan walikuwa wanaishi naye karibu, ingawa hali ya nyumbani kwao ilikuwa ngumu ila Noela hakujali kwasababu alimpenda sana. Jonathan ni yatima, wazazi wake wote walikufa kwa UKIMWI. Lakini katika huo mtaa wao wengi hawakujua hilo hata Noela naye hakujua. Jonathan alijua kilichowaua wazazi wake.

Noela alimpenda sana Jonathan lakini Jonathan alikuwa muhuni sana. Noela alijikuta akijiingiza kwenye dimbwi la mapenzi na kufanya ngono zembe bila kutumia kinga.

Siku zilivyozidi kwenda uhusiano waoulionekana kuwa mzuri. Siku moja Noela akiwa mezani anakula pamoja na wazazi wake mara akaanza kujisikia vibaya akaanza kutapika, kwa kuwa wazazi wake walimpenda walimpeleka hospitalini haraka.

Mzee Briton; Daktari mwanangu anaumwa sana

Daktari; Hamna shida hapa atapona tu, ngoja tuchukue vipimo

[Majibu yalivyotoka]

Daktari; Mzee mwanao anaonyesha ni mjamzito na pia ameathirika kwa virusi vya UKIMWI!!

Mzee Briton; Mungu wangu!!

Kwa bahati mbaya mzee Briton alipoteza maisha hapohapo baada ya kupata mshtuko mkubwa sana. Noela aliruhusiwa kurudi nyumbani na majibu yake lakini hakujua kilichompata baba yake. Noela alipofika nyumbani alimkuta mama yake amekaa kibarazani, akampa mama yake yale majibu ya hospitali alishtushwa sana na majibu yale. Noela bado hakuyajua yale matokeo lakini aliyajua baada ya mama yake kumuuliza ndipo akagundua kuwa ni muathirika wa gonjwa la UKIMWI na tena ana mimba ya utotoni kwa kuwa alikuwa na miaka 16 [kumi na sita].

Baada ya kugundua hilo aliienda kwa Jonathan na kuongea naye na alipofika akamwambia kuwa ana mimba. Jonathani alimkana na kumwambia kuwa asimjue na akamfukuza ndani ya nyumba yake aliondoka na kuelekea nyumbani kwao. Ndipo alikuta umati wa watu nyumbani kwao alipouliza aliambiwa kuwa baba

## .......WANAFUNZI "TUBADILIKE", SUBIRI MAPENZI YANA WAKATI WAKE!!

kuwa baba yake amefariki kwa presha baada ya kupata majibu yako na mama yako yupo hospitali alipoteza fahamu baada ya kupata taarifa ya msiba.


Noela alilia sana na kujutia kwa yote aliyoyafanya wakati alipokuwa shuleni amepoteza masomo na maisha yake yalianza kuwa magumu.Alitunza ujauzito wake na kufanikiwa kujifungua salama mtoto wa kike aliyeitwa Brenda.Noela alimpenda sana mwanae na alimlea katika maadili mema na hakutaka mwanae aharibikiwe na alimwambia asome kwa bidii sana asifuate makundi mabaya.

Ndipo mama yake aliruhusiwa kurudi nyumbani aliishi na mwanae vizuri.Wadogo zake Noela waliendelea kusoma na kufanya vizuri darasani.

Noela alianza kushambuliwa na magonjwa nyemelezi kama vile kukohoa,kutapika na kuharisha.Walimpeleka hospitali na kupewa dozi ya [ARV] ili imsaidie kurefusha maisha na wakampa ushauri kuwa anatakiwa kula chakula bora na chenye lishe.

Maisha yao yalikuwa sio mazuri sana yalikuwa ya kawaida kwasababu mama yao alikuwa hana kazi nzuri sana na kazi yake ya kuuza duka yaliweza kukidhi maisha na alijitahidi mwanae apate lishe bora na alirejea katika hali yake ya kawaida na kuanza kunenepa kwa kuwa alikuwa na mvuto, baadae aliamua kuusambaza virusi vaya ukimwi makusudi na kila alipokuwa akikutana na mwanaume alitembea nae bila kutumia kinga. Baada ya muda Noela aliugua na kufariki dunia kwa kuwa alipodhani anausambaza ugonjwa alikuwa akiongeza kiasi cha virusi kwenye damu yake, na mwanae Brenda akafata nyayo za mama yake za tabia mbaya sana na sasa ana maambukizi nayeye na anaishi na bibi yake.

**IMEANDALIWA**
**MONICA, DORICE NA GLADY**
**KINDOROKO SEKONDARI**



# MADHARA YA UGONJWA WA UKIMWI KATIKA MASOMO!

Mimi ni mwanafunzi wa shule ya sekondari Kihurio kidato cha nne mkondo wa sayansi, nina umri wa miaka kumi na nane. Nina masikitiko makubwa sana kwani nikiwa darasa la pili nilifiwa na wazazi wangu kwa ugonjwa hatari wa ukimwi.Nikiwa mtoto pekee wazazi wangu waliniacha katika wakati mgumu kwani niliwazoea sana kwa mapenzi yao.

Nilimaliza masomo yangu ya msingi katika hali ngumu kwani nilikosa hata hela ya kununua madaftari, kalamu na hata sare za shule.Lakini pamoja na hayo mungu akanijalia nikafaulu na kuanza masomo ya sekondari hadi sasa ninapozungumzia haya nipo kidato cha nne.Nawashukuru walimu wangu pamoja ndugu zangu kwa ujumla kwa kushirikiana na mimi japokuwa ni yatima wameniwezesha kupata elimu ili nipunguze ugumu wa maisha yangu ya baadae.

Katika maswala ya kujisomea usiku hali ilikuwa ni ngumu kwa sababu ninaishi na bibi na mama yangu mdogo nikiwa na mtoto wa mama mkubwa kwa jina ni Hidaya na mtoto wa mama mdogo kwa jina ni Kassimu. Tunaishi kwa kutegemea kilimo na biashara yetu ya kahawa lakini kipato anachopata bibi kwenye hiyo biashara hakikuwa kinatosha kwa sababu kila kitu kinategemea biashara hiyo.Kwa hiyo wakati mwingine sisomi kwa sababu bibi anabanwa hadi fedha ya kununulia mafuta ya taa haipatikani.

Si hayo tu bali yapo mengine kama vile kalamu, madaftari nakosa hela yakununua hadi inanilazimu mimi kujishughulisha na biashara ndogondogo kama vile kuuza ubuyu kwa wanafunzi wenzangu kashata za karanga,mikate ya kumimina ili tu nipate fedha ili niweze kusaidia bibi japokuwa nipo nje ya uwezo wangu.

Pamoja na hayo yote kuna mahitaji mengine kama vile chakula kutopatikana hadi kunipelekea kujishughulisha na kilimo hadi siku nyingine nashindwa kwenda shuleni ili niweze kwenda shambani. Kwa sababu ninaishi na bibi yangu na amepata matatizo ya moyo tangu alipofiwa na mtoto wake kwa sababu ndiye aliyekuwa anamtegemea kwa kila kitu.

Kwa ujumla matatizo haya yamesababisha mimi na familia yangu niliyoachwa nayo tunaishi maisha ambayo si mazuri na pia katika masomo yangu kwa sababu siku nyingine nachelewa vipindi darasani na nakuta wenzangu wanamalizia vipindi.

Mwisho napenda kutoa ushauri kwa wanafunzi wenzangu na wazazi wanapaswa kujikinga na kupambana na maambukizi ya virusi vya UKIMWI, na pia kwa wale ambao wameondokewa na wazazi wao kama mimi wasikate tamaa, pia nashauri mashuleni tusiwatenge wanafunzi ambao wazazi wao wamepoteza maisha kwa ugonjwa hatari wa ukimwi. Napenda kutoa shukrani kwa wanafunzi wenzangu wa kidato cha nne sayansi kwa kunipa ushirikiano wa biashara zangu nilizokuwa nazifanya na kuniwezesha mimi kutoonekana kama mtoto yatima. Wapo baadhi nao ni Tabu, Amina , Nanzia, Sirieli na Mariam Seng'enge.

**Imeandaliwa na:**
**Hajra Omary**
**Kidato cha Nne**
**Kihurio Sekondari.**



**Ukimwi unaua!**

**Vijana Tuweni Makini!!**

# KISA MKASA CHA MFANYAKAZI WA NYUMBANI

Familia ya Bwana Selemani na mkewe Sarah wana mtoto mmoja wa kiume aliyeitwa Shabani, walikuwa wanaishi Magomeni jijini Dar es salaam. Maisha yalikuwa mazuri kwani baba alikuwa mwajiriwa na mama yake alikuwa anajishughulisha na biashara ndogondogo hivyo waliweza kumsomesha mtoto wao.

Kutokana na maisha kuendelea kuwa mazuri mama Shabani aliamua kumtafuta msaidizi wa pale nyumbani ili aweze kushughulikia vizuri biashara yake. Ndipo alipokubaliana na baba Shabani aende kijijini kwao huko Tanga akamtafute huyo mfanyakazi.

Mama Shabani akajiandaa akaenda kwao Tanga akawaeleza wazazi wake kilichomleta. Kesho yake asubuhi mama yake mama Shabani akamletea mtoto ambaye ni yatima kwani wazazi wake walikufa kwa UKIMWI hivyo na yule mtoto naye alikuwa ameambukizwa, mama Shabani akaelezwa yote lakini kwa kuwa alimuhitaji kwa hamu ikabidi amchukue hivyohivyo na kwenda naye Dar es salaam. Walipofika mama Shabani hakumtambulisha kwa undani sana bali aliwatajia jina tu kuwa anaitwa Jenifa.

Maisha yakaendelea kadri siku zilivyozidi kwenda Jenifa hali yake ikawa inabadilika taratibu lakini mzee Selemani akaanza kumtaka kimapenzi lakini Jenifa akakataa kabisa, Mzee Selemani akamwambia atamfukuza kazi lakini Jenifa alibaki na msimamo wake. Jumamosi mzee Selemani yupo nyumbani haendi kazini kwasababu ni siku ya mapumziko lakini mke wake yeye hana siku ya kupumzika kwasababu amejiajiri mwenyewe. Majira ya mchana Jenifa alikuwa amepumzika chumbani kwake mara akasikia mlango ukifunguliwa taratibu akashtuka kuangalia mzee selemani ashafika ndani, Jenifa akaogopa sana akataka kukimbia ila mlango ulifungwa na funguo zimewekwa mfukoni akataka apige kelele lakini akaambiwa ukipiga kelele tu ni lazima nikuue basi Mzee Selemani akafanikiwa kumbaka. Jenifa akaachiwa maumivu makali mno lakini hakusema kwa mtu. Jenifa hakusema kwa mtu yeyote yule hivyo ikawa ni siri yao.

Siku zikapita maumivu yakakoma Jenifa akawa amepumzika sebuleni kwenye kochi, wazazi wote walikuwa kazini. Mara mlango ukafunguliwa akashtuka lakini kuangalia kumbe alikuwa Shabani basi ile hofu ikaondoka lakini kwa kuwa alishtuka sana usingizi ukakata akawa amekaa tu palepale kwenye kochi. Shabani aliwahi kutoka shule ili amshawishi Jenifa wafanye mapenzi lakini Jenifa akakataa ila jibu lake halikuingia kichwani kwa Shabani. Siku zikapita Shabani akaendelea kumshawishi lakini alipoona amekuwa na msimamo akaamua kumuingilia kwa nguvu na kumsababishia maumivu. Jenifa hakusema kwa Sara jambo hilo, ndipo nikakumbuka kwamba "mtoto wa nyoka ni nyoka," ila hawakujua ukweli kuhusu Jenifa.

Siku moja mama Shabani alikaa na familia yake na kuamua kuwaambia ukweli kuwa Jenifa alimtoa kijijini ni yatima wazazi wake walikufa kwa ugonjwa hatari wa ukimwi. Kabla hajamaliza mumewe akanyanyuka kwa mshangao, Sara akasema ndio nina ukimwi mzee Sulemani akaanza kusema mke wangu mimi ninao na Shabani naye hivyo hivyo, Sara akawauliza kwa hiyo mmefanya ngono na Jenifa? kwa hasira Sara akaamua kuondoka kwenda kwao Tanga.

Na hapo ndipo familia ikavunjika na sasa mzee Sulemani haijulikani alipo na Shabani anatangatanga hajui pa kwenda,Jenifa naye aliamua kurudi kwa Tanga na sasa anatumia vidonge vya kurefusha maisha [ARV].

**IMEANDALIWA NA:**
**JOSEPH G MSOFE**
**KIDATO CHA TATU**
**NGUJINI SEKONDARI**

## UKIMWI HUU!!WATOTO WANATESEKA- KISA CHA KWELI

Kulikuwa na familia ya watu wa nne, familia hiyo ilikuwa na baba pamoja na mama, baba Anoldi na mama Vailet na watoto wa kike wawili wa kwanza alikuwa Martha wa pili na wa mwisho alikuwa Winfrida. Familia hii ilikuwa na upendo na amani,baba wa familia hii alikuwa anafanya kazi kiwandani na mama wa familia hii alikuwa anauza vitenge. Martha alikuwa akisoma kidato cha pili na Winfrida darasa la tatu. Waliishi vizuri na walikuwa wanapendana sana hadi majirani wakawa wanawaonea wivu,siku moja kazini kwa Anold kulitokea wizi wa hela na bosi wa kazini hapo alipochunguza alijulikana kuwa Anold ndiye aliyeiba pesa hizo kwa hiyo adhabu aliyopewa ni kufukuzwa kazi na hakupewa hata pesa zake aizokuwa anadai kazini.

Akaamua kumweleza mke wake na hatimaye mkewe akamwelewa wakaishi kwa shida sana maana yule mama ndiye alikuwa kama baba pale ndani.Kila kitu kilimwangalia yeye kuanzia asubuhi hadi usiku, chakula na ada za watoto wao. Hatimaye akamaliza hadi msingi wa biashara yake.Siku ya siku akawa hana kazi wakawa siku nyingine wanakula hata mlo mmoja na kila kukicha afadhali ya jana. Anold akaamua kutafuta kazi,alijaribu kuzunguka huku na kule lakini hakupata mafanikio. Siku moja alikwenda kutafuta kazi kwenye kiwanda kimoja na alimkuta bosi ambaye alikuwa ni mama wa miaka kama 49, yule mama alikubali kumpa kazi ila kwa masharti kuwa ashirikiane nae kingono na yule baba kwa sababu alikuwa na shida alikubali kuwa na mahusiano na bosi wake.Ilipofika kesho yake akaanza kwenda kazini baada ya siku kadhaa maisha yake yalianza kubadilika yakawa mazuri hata kuliko ya mwanzo.

Familia yake ilimshukuru Mungu kwa baba yao kupata kazi. Anold aliendelea na mahusiano na bosi wake kadiri siku zilivyozidi kwenda mapenzi yao ndivyo yalivyozidi kupamba moto. Hakufahamu kuwa bosi wake alikuwa muathirika wa virusi vya UKIMWI,baada ya miezi kadha Anold alianza kuwa na hali mbaya alianza kuumwa kifua na kuwa na utando mdomoni na alipungua uzito sana. Familia yake ilimshangaa sana na majirani mpaka mke wake akaamua kumuuliza kuwa ana tatizo gani hakuwa na jibu sahihi kwani alikuwa hajapima afya yake.Baada ya siku kupita hali yake ilizidi kuwa mbaya akaamua kwenda kupima afya yake,akapima baada ya muda kidogo majibu yakawa tayari akaitwa kwenda kuchukua majibu yake, alipofika akaambiwa ukweli kuwa ameathirika alihuzunika na alilia sana pia alijuta kwanini hakuwa mwaminifu kwa mke wake.

Akaamua kwenda kwa bosi wake ambaye ni mke wa nje ya ndoa alipofika alikaribishwa vizuri akaanza kumweleza kuwa ameathirika na alidai inawezekana aliyemwambukiza ni bosi wake. Hatimaye yule bosi akabadilika ghafla na kumtukana kisha akamwambia hujui hapa mjini siwezi kufa peke yangu nitakufa bali na wewe pamoja na mwenzako watanifuata na ukitaka na wewe kufa na wako, halafu naomba utoke kwangu sikujui". Basi Anold akaamua kuondoka huku machozi yakimtoka,alipofika nyumbani hakumweleza mke wake kitu chochote bali aliamua kumficha.

Mke wake alipomhoji alimdanganya akamwambia kuwa anahuzuni amefukuzwa kazi, mke wake alihuzunika sana pamoja na watoto wao na hatimaye shida na ugumu wa maisha ukachukua nafasi tena katika familia ile.

Baada ya miezi ya mitatu na nusu Anold alikuwa na hali mbaya zaidi na akawa na mkanda wa jeshi hapo ndipo mkewe ilipogundua kuwa mume wake inawezekana ameathirika akaamua kumhoji taratibu.

Siku moja mama yake Martha alikuwa anaongea na mume wake ndipo akaamua kumuuliza, na mume wake akashindwa kuvumilia na kupiga moyo konde akaamua kumpasulia mke wake.

## ....UKIMWI HUU!!WATOTO WANATESEKA- KISA CHA KWELI

Mke wake alilia sana kwani alijua na yeye atakuwa ameathirika, pia alimlaumu sana mume wake kwanini aliamua kumsaliti hivyo!. Lakini baada ya muda wakaamua kusameheana. Siku zilizidi kwenda na hali ya Anold ilizidi kuwa mbaya na hatimaye akaaga dunia, lakini ilikuwa ni pigo kubwa sana kwenye hii familia. Baadhi ya watu waligundua kuwa Anold amefariki kwa ugonjwa wa ukosefu wa kinga mwilini hivyo wakaitenga familia ya bwana Anold. Baada ya msiba kuisha mama yake Martha akaanza naye kuugua mara kifua, homa za mara kwa mara, vidonda mdomoni na mwisho akapata kifua kikuu pamoja na mkanda wa jeshi na hatimaye akapoteza maisha. Martha na Winfrida walilia sana wakashirikiana na wasamaria wema wakamzika mama yao. Msiba ukaisha maisha yao yakawa magumu zaidi na kila walipokanyaga hapakanyagiki, na walipokuwa wanatafuta msaada walikosa na walitengwa na jamii. Siku zikapita ndugu wa Anold wakaanza kufuatilia mali za ndugu yao kwa madai ya kutaka kuwasaidia wale watoto na hatimaye wakashinda wakauza mali zote na wakaanza kugawana hela.

Martha na Winfrida wakawa hawana mahali pa kukaa, wakajiona hawastahili kuishi tena duniani, wakaona bora wangetangulia wao kuliko maisha wanayoishi sasa ya shida na dhiki.

Mungu si athumani wakapata msamaria wakachukuliwa wakaenda kulelewa kwenye kituo cha watoto yatima wakapata hifadhi na hatimaye wakaweza kuendelea na shule.

Walimshukuru Mungu sana na maisha yao yakabadilika kwa kiasi japokuwa walikuwa na pigo ambalo ilikuwa ni vigumu kwao kusahau.

**Imeandaliwa na:**
**Florah Harold Minja,**
**Kidato cha Tatu**
**Kindoroko Sekondari.**



# HIV/AI



KLABU YA KINDOROKO SEKONDARI



KLABU YA VUDEE SEKONDARI WAKIELIMISHA MASWALA YA UKIMWI KWA NGOMA



Mkuu wa Idara ya Afya na Ukimwi, Paul Nyindo akitoa somo kuhusu maambukizi ya VVU/Ukimwi.



KLABU YA NGUJINI SEKONDARI



KLABU YA MVURE SEKONDARI,5) KLABU YA KINDOROKO WAKIFIKISHA UJUMBE WA UKIMWI KWA NYIMBO



KLABU YA VUDEE SEKONDARI

# DS CLUBS



KLABU YA NGUJINI SEKONDARI



KLABU YA JITENGENI SEKONDARI



KLABU YA KIHURIO SEKONDARI



KLABU YA KWANGU SEKONDARI



KLABU YA KINDOROKO WAKIWA KWENYE MAFUNZO YA UKIMWI



KLABU YA KIGONIGONI SEKONDARI

# ASIYESIKIA LA MKUU..!!

Kulikuwa na dada mmoja jina lake aliitwa Juliety, alikuwa anaishi Magomeni jijini Dar es Salaam. Aliishi na mama yake na kaka yake aliyekuwa anaitwa Baraka, nyumbani kwao walikuwa maskini sana.Baraka alikuwa anafanya kazi ndogo ndogo za mtaani ili waweze kupata mahitaji muhimu  lakini Juliety kila siku alikuwa anatoka asubuhi na kurudi usiku na anarudi akiwa amelewa.

Siku moja Baraka akamwambia Julieth “sikiliza nikuambie ndugu yangu achana na hiyo tabia ya ulevi ujue ulevi ni mbaya na hauna faida yoyote” lakini Julieth akamjibu Baraka kuwa aachane na maisha yake kwa sababu hela anazotumia kununulia pombe sio za kwake na akamwambia amwache kama alivyo. Baraka akamwacha hakuendelea kumsemesha nae, Juliety akaendelea na tabia yake ya ulevi na mara nyingine alikuwa analala hukohuko kwa wanaume. Mama yake Juliety akamwonya mwanae lakini bado Juliety hakusikia. Siku nyingine tena mama yake Juliety alivyoona tabia ya mwanae inazidi kuwa mbaya zaidi akaamua kumuonya na kumwambia asipoangalia atakufa kwa UKIMWI kwa kuwa sikio la kufa halisikii dawa basi Juliety aliendelea na tabia yake. Baadaye Juliety akaamua kutoroka na kwenda kuishi na mwanaume aliyekuwa anaitwa Omari kisa ana pesa akaamua kumuacha mama yake na kaka yake waendelee kuishi maishi yao ya kimaskini.

Siku zikazidi kwenda Baraka akaajiriwa kwenye kiwanda cha pepsi, maisha ya pale kwao yakabadilika na hatimaye Baraka akaamua kujenga nyumba ili aishi na mama yake. Maisha aliyoishi Baraka na mama yake yalikuwa ya furaha na ya amani. Kwa kuwa uchungu wa mwana aujuaye mzazi basi mama yake Juliety alikuwa anamkumbuka sana mwanaye lakini hakufanikiwa kujua ameenda wapi. Lakini baada ya miezi saba kupita Juliety akafukuzwa na yule mwanaume aliyemtorosha kisa kapata mimba. Basi Juliety akawa na maisha magumu mno hana pakulala wala pakula. Siku moja Juliety akaanza kutafuta kazi za ndani, mara akaenda kwao lakini yeye hakujua ni kwao kwasababu ile nyumba ni mpya.Juliety alivyogonga akafunguliwa na msichana wa kazi akakaribishwa ndani akaomba maji ya kunywa, alivyokuwa anaendelea kunywa maji mara akamuona mama yake ametoka kuoga. Juliety alivyomuona tu mama yake akaanza kulia na kumuomba mama yake msamaha, mama yake hakusita akamsamehe akawa anaishi naye. Jioni kaka yake akatoka kazini akamkuta Juliety anaongea na mama yake, Baraka akafurahi sana kumuona ndugu yake amerudi.

Baada ya Juliety kupumzika akaanza kuwaelezea jinsi maisha yake yalivyokuwa huko alipokuwa anaishi na mateso aliyoyapata. Baada ya kusimulia kaka yake alimuonea huruma na mama yake alilia sana. Basi wakamshauri aende hospitali ili aanze kliniki kama kawaida ya mama mjamzito. Kesho yake akaenda kliniki akapimwa ukimwi na kuchekiwa kuwa mimba ina miezi mingapi. Juliety alikutwa ana virusi vya ukimwi na mimba ilikuwa ina miezi minne. Daktari akampa ushauri jinsi ya kuishi ili mtoto asiambukizwe virusi vya ukimwi. Juliety alilia sana akaenda kuwataarifu ndugu zake basi kaka yake akamshauri atumie vidonge vya ARV, Juliety akakubali bila ubishi wowote. Juliety alifunzwa na ulimwengu hakutaka afunzwe na mamaye. Basi Juliety akaishi na ndugu zake bila kutengwa wala kunyanyaswa mpaka alipojifungua mtoto wake wa kike akamwita jina la mama yake yaani Jaklini. Hivyo Juliety anaishi na ndugu zake mpaka sasa huko Magomeni jijini Dar es salaam.

Imeandaliwa na:
Magdalena J. Msuya

# VIJANA TUONGEE! ANTI SUZY YUPO KUWASIKILIZA NYIE



Mpendwa Antie Suzy,
Kwanini ukiangalia movie za X unaweza kupata hamu ya kujamiiana na msichana?
JOHN N. MSUYA
VUDEE SEC SCHOOL

***Tukumbuke kuwa mwili wa mwanadamu uongozwa na milango mikuu ya fahamu kama kugusa, kuona, kuonja, kunusa na kusikia kwa kupitia milango hii taarifa upelekwa kwenye ubongo kuwa mtu huyu yupo tayari kwa jambo gani.***

***Hivyo katika kujamiiana kama matendo mengine uongozwa au utawaliwa na milango mikuu ya fahamu kama kugusa, kuona, kunusa na kusikia ambayo huamsha hamasa/hisia kwa ajili ya tendo hili, na hamasa/hisia hizi huweza kuamshwa kwa kuangalia picha za utupu, movie za ngono na kusoma majarida yaliyo na story za ngono n.k baada ya kuangalia picha, kusoma au kusikia story, movie za ngono taarifa upelekwa kwenye ubongo ili kukuandaa kwa tendo la kujamiiana.***

***Ni sawa na ukitaka kula unapoona tu chakula taarifa upelekwa kwenye ubongo kuwa unu njaa ndipo urudishwa na tezi za mate mdomo utoa mate kwa ajili ya kula.***

***Hivyo Mdogo wangu jitahidi kuepuka kuangalia movie, picha na kusikiliza story hizi za ngono ili kuepukana na ngono zisizo salama za umri mdogo, kuna madhala mengi yatokanayo na ngono za umri Mdogo kama magonjwa ya zinaa, magonjwa ya njia ya mkojo, UKIMWI na mimba zisizotarajiwa ambazo zinaweza kukuhalibia malengo ya maisha yako.***

Mpendwa antie Suzy
Malaria huenezwa kwa njia ya kung'atwa na mbu endapo mbu ametoka kufyonza damu ya mtu mwenye malaria na kisha kupelekea kwa mtu ambaye hajaathirika na ugonjwa wa malaria. Sasa basi kwanini wanasayansi hudai kwamba ugonjwa wa UKIMWI hauenezwi kwa njia ya kungatwa na mbu?
GHUHENI Y. MGANGA
VUDEE SEC SHOOL

***Kwanza VVU ili waweze kuzaliana na kuishi kwenye mwili wa mnyama yoyote ni lazima vishambulie chembe hai nyeupe za kinga ya mwili hivyo haviwezi kuishi kwenye mfumo wa damu wa mbu kwa sababu hana chembe hai nyeupe za kuwezesha VVU kuzaliana. Kwa maana hiyo mbu anapomuuma mtu mwenye virusi vya ukimwi, virusi hivyo hufa mara moja kwa sababu Virusi vya Ukimwi vinaweza kuishi kwenye mfumo wa damu ya binadamu au mnyama mwenye mfumo wa damu sawa na binadamu mfano Sokwe au nyani.***

***Pia kwenye mfumo wa mmengenyo wa chakula wa mbu kuna vimengenyo kwenye mrija wa mbu ambavyo huviua virusi mara moja vinapofyonzwa.***

Mpendwa antie Suzy
Kuna ukweli gani endapo mtu atakaa zaidi ya miaka kumi na tano baada ya kubalehe bila ya kujamiiana kwani kwenye kujamiiana kuna usemi usemao mtu akikaa miaka kumi na tano bila ya kujamiiana anaweza akachanganyikiwa ?
GABRIEL M. STEPHANO
VUDEE SEC SCHOOL

***Kuamua kukaa kwa miaka kumi na tano (15) au na zaidi bila kufanya ngono hutokana na uhamuzi na malengo ya mtu binafsi na ni njia nzuri ya kujilinda kipindi cha kukuwa(kubalehe) kwa vijana na inawezekana ukiamua.***

***Vile vile kutofanya ngono kwa muda mrefu hakuna uhusiano na mtu kuchanganyikiwa, kwani mtu huchanganyikiwa utokana na sababu nyingi za kisaikologia kama msongo wa mawazo au mshtuko uliozidi kipimo na kusababisha ubongo/ufahamu wa mtu kushindwa kuvumilia misukosukao ya maisha, hivyo kupoteza ufahamu au kuchanganyikiwa kunaweza tokana na uhasilia wa taarifa ya kuchanganyikiwa katika familia yako ambayo upatikana kwenye vibeba taarifa vya binadamu (DNA) na msongo wa mawazo na si kwa kutofanya ngono kwa muda mrefu.***

Mpendwa antie Suzy
Je! VVU vinakuwepo wapi katika vina vya uzazi wa binadamu? Maana tumekuwa tukielezwa na kusoma kuwa VVU huwa kwenye maji maji na wakati mwengine kwenye damu na inakuwaje wapenzi au hata mwanandoa mmoja anaweza kuwa ameathirika mwingine yuko salama
YUSUPH A. KAMLEKA
NGUJINI SEC SCHOOL

## VIJANA TUONGEE! ANTI SUZY YUPO KUWASIKILIZA NYIE

***Asante kwa swali zuri sana, ni kweli VVU ukaa kwenye maji maji ya mwili kama maziwa ya mama anaenyonyesha, damu , maji maji ya vina vya uzazi kama ute wa ukeni na ute unaozunguka mbegu za kiume.***

***Virusi vya Ukimwi vinapoingia kwenye mwili wa binadamu kupitia kidonda au michubuko yoyote mtu aliyonayo huenda moja kwa moja na kuvamia aina ya chembe hai nyeupe za kinga ya mwili ya mwanadamu ( T- helper lymphocytes au CD4+ lymphocytes) ambapo hapo VVU upigana na kuziua kinga za mwili kwa kuzaliana zikichukua umbo na mfumo sawa wa chembe hai nyeupe za kinga ya mwili ya mwanadamu.***

***Ndo maana imekuwa vigumu sana kupata chanjo ya Virusi vya Ukimwi kama ilivyopatika-na chanjo ya virusi vya magonjwa mengine kama Pepo Punda na Ndui kwa sababu VVU uchukua mfumo sawa na chembe hai nyeupe za kinga ya mwili ya mwanadamu ( T- helper lymphocytes au CD4+ lymphocytes)ivyo ukitengeneza chanjo ya kuua VVU ni sawa na kuua chamber hai nyeupe ya kinga ya mwili ya mwanadamu kwasababu zinafanana.***

***Na muda unavyozidi kwenda mbele tangu VVU vianze kushambulia chembe hai nyeupe za kinga ya mwili ya mwanadamu, kinga ya mwili ya mwanadamu hushuka au kuisha kabisa ndipo tunasema mtu huyu ana UKIMWI(Upungufu wa KInga MWIlini) ikimaanisha kinga yake ya mwili imeshambuliwa sana na VVU kusababisha mwili wake kukosa kinga ya kumlinda na magonjwa shambulizi kama TB, Mkanda wa Jeshi, mafua ya mara kwa mara, Homa /Malaria, Kuharisha na n.k.***

***Hivyo kujibu swali lako mtu yoyote ataambukizwa VVU endapo tu kutakuwa na mgusano wa maji maji ya mwili yaliyotajwa na mchubuko au kindonda mtu ambacho anacho kama hilo halitatokea basi maambukizi kupatikana ni vigumu na taarifa za wapenzi au hata mwanandoa mmoja ameathirika mwingine yuko salama ni chache sana kutokana na maumbile ya vina vya uzazi kuwa laini sana, na sana sana kwa wanawake kwani wao hukaa na ute wa mbegu kwa muda mrefu kwenye maumbile yao hivyo huwafanya kuwa katika hatari zaidi ya kupata maambukizi kuliko wanaume.***

Mpendwa antie Suzy
Nina swali langu ambalo kila siku nilikuwa nikilifikiria bila kupata jibu lake. Eti mtu yoyote ambaye ukimtekenya anaposhtuka ni ishara tosha kuwa huyo mtu hafanyi ngono?

Tatizo langu lingine ni kwamba mimi ninapokaa darasani kwa muda mrefu hata kama sijafikiria maswala ya ngono mwanajeshi wangu anasimama je nifanyaje?
RAMADHANI OMARY
JITENGENI SEC SCHOOL

***Kumtekenya mtu na kushtuka haina uhusiano wowote na mtu kutofanya ngono, hii inausiana na viamsha hisia tu vilivyopo kwenye mwili wa mtu kulingana na maumbile ya mtu binafsi, na huna maamuzi ya jinsi gani ya kuvizuia hivyo uwezi kupima kuwa mtu hajafanya ngono kwa kumtekenya hiyo ni siri ya mtu binafsi.***

***Kwa kijana ulie balehe mwanajeshi wako kusisimama ni kitu cha kawaida na inaonesha kuwa wewe ni rijali, na ndo maana mara nyingi vijana ambao ndio wanabalehe upata ndoto nyevu na ujikuta asubuhi wamechafuka hivyo huna sababu ya kuwa na wasiwasi siku zinavyozidi kwenda hali hiyo itapungua.***

***Cha muhimu kufanya wakati unaona hali hii jitahidi kufikiria kitu kingine au fanya jambo litakalo kusaidia uondokane na hali hiyo .***



# KILIO CHA MSHUMI

Mshumi ni binti ambaye alibahatika kuishi na wazazi wake wote wawili huko Minazini wilayani Same. Lakini ndugu zake walikuwa wanaishi jirani na mji wao ambao ni Jitengeni. Baada ya miaka michache Mshumi alipofikisha umri wa miaka mitano mama yake alifariki dunia kwa ugonjwa wa shinikizo la damu. Hivyo ikamlazimu baba yake Mshumi kumpeleka mwanaye akaishi na babuna bibi yake huko Jitengeni, yeye akaenda kutafuta maisha mjini.

Mshumi alipendwa sana na babu na bibi yake hivyo alidekezwa sana. Na baada ya miaka miwili Mshumi alijiunga shule ya msingi hapo Jitengeni na baadaye akamaliza elimu ya msingi. Matokeo yalivyotoka Mshumi alibahatika kuchaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari shule ya Mvurekongei. Baada ya kujiunga Mshumi alijitahidi katika masomo yake na alipofika kidato cha pili alipata marafiki wakike watatu nao ni Chausiku, Bikashi na Rebeka. Mshumi akapata rafiki wa kiume aliyeitwa Hatibu. Alimpata rafiki huyu kutokana na kushindwa vishawishi toka kwa rafiki zake wa kike. Rebeka alikuwa ameathirika lakini hakujua wala rafiki zake hawakujua.

Siku moja katika maandalizi ya sikukuu ya krismasi na mwaka mpya waliamua kwenda kijiji cha jirani kiitwacho Mabambara kwa msusi aitwaye Pamela.

Wali kwenda kwa msusi ili wat-obolewe masikio pua na kusukwa,akaanza kutobolewa Chausiku akifuatiwa na Bikashi akaja Rebeka mwishowe Mshumi. Kutokana na uhaba wa elimu aliokuwa nao yule msusi aliwatoboa masikio na pua kwa kutumia sindano moja. Hivyo Mshumi alipata ugonjwa wa ukimwi bila ya yeye kujijua.

Kwa kuwa Mshumi hakujua kuwa yeye ni mwathirika hivyo akaenda kufanya mapenzi na yule rafiki yake wa kiume [Hatibu]bila ya kutumia kinga. Hatimaye Mshumi akapata mimba na Hatibu akapata maambukizo ya virusi vya ukimwi bila ya wao kujijua, maendeleo ya Mshumi darasani yakaanza kuwa mabaya.Baada ya miezi mitatu hali ya Mshumi ikaanza kuwa mbaya magonjwa yasiyo kwisha,hivyo bibi yake akaona ni vyema ampeleke hospitali.Kabla ya kufika hospitali bibi akamwambia Mshumi unajua huku kuumwa ni dalili ya kuwa wewe ni mjamzito, Mshumi akashtuka na kumwambia bibi yake kama nitaonekana ni mjamzito nitajua basi bibi akashikwa na uoga na hofu kubwa lakini alimbembeleza. Walipofika hospitali bibi akamwambia daktari kuhusu hali halisi ya Mshumi kwamba "akijikuta ni mjamzito atajiua"daktari akamsikiliza bibi kisha akaanza kumpima Mshumi. Vipimo vikaonyesha Mshumi ni mjamzito na ameambukiza virusi vya ukimwi, daktari akamwambia bibi na Mshumi kwa pamoja wote wakaangua kilio. Daktari akawanyamazisha na kumsihi Mshumi asijiue na akampangia tarehe ya kuja hospitali kupata huduma ili aishi kwa matumaini na hapo ndipo Mshumi akaacha masomo kabisa.

Baba yake Mshumi alipozipata zile taarifa ilikuwa ni kasheshe, alisema kwa hasira…"siku na mahali popote haijalishi kunanini nitamwua Mshumi kwani nimepoteza fedha zangu nyingi,ni heri angesema mapema kuwa hatasoma". Lakini ndugu wa familia ile walikaa kikao cha ndugu na kusuluhisha ule ugomvi.Siku moja baba yake Mshumi alikuwa anakwenda shambani asubuhi kufukuza nyani na tumbili wasile mahindi, bibi naye alikwenda porini kutafuta kuni.Hivyo Mshumi alibaki nyumbani peke yake wakati bibi yake akiwa porini alichomwa na mwiba kwenye kidole cha katikati cha mkono wa kulia.Na huku nyumbani Mshumi alishikwa na uchungu wa kujifungua hapo ndipo mambo yalikuwa magumu kwa Mshumi tumbo lilimuuma hadi majira ya

## .......KILIO CHA MSHUMI

saa tano, kwa bahati nzuri bibi yake aliweza kurudi nyumbani.

Wakati bibi anaingia ndani alishtuka kumkuta Mshumi amelala kitandani analia na kuomba msaada, bibi aliingiwa na woga lakini alijikaza kisabuni na kumsaidia mjukuu wake kumzalisha kwa sababu bibi alikuwa mkunga akafanikiwa kumzalisha.Bila ya kujua kuwa alikuwa na kidonda kwenye kidole na wala hakuvaa kizuizi chochote mkononi [gloves] hivyo bibi naye akaambukizwa vvu bila yeye kujijua. Mshumi akafanikiwa kujifungua mtoto wa kiume akampa jina la Kisuse kwa sababu Mshumi hakuwa na elimu juu ya ukimwi.

Nyumba nzima wakaanza kuumwa ikawa hakuna hata wa kumjulia mwenzake hali nyumba ikageuka ikawa kama wodi ya wagonjwa wa kipindupindu hivyo akamnyonyesha mwanae bila kujua na mwanae naye akapata ugonjwa wa ukimwi. ndugu zao wote wakawatelekeza hata salamu hawakupewa.

Walichofanyiwa chema walitafutiwa mfanyakazi wa kuwasaidia,yule mfanyakazi naye pia hakuwa na elimu kuhusu ugonjwa hatari wa ukimwi.

Hakujua namna gani ya kuwahudumia wagonjwa wakutumia vifaa kama [gloves] naye ukimwi aliwahudumia bila ya akapata maambukizi.

Pale ndani pakawa hapana msaidizi na ndugu zao hawakuwajali tena,waliendelea kuumwa na kudhoofika ikabidi vyombo vya usalama [polisi] waingilie kati na kuwapeleka hospitalini kwa ajili ya matibabu zaidi.

MAAMBUKIZI YANAWEZEKANA KWA MTU YEYOTE, TUSIDHARAU TUBADILIKE!

ATHUMANI D. ATHUMANI,
MVUREKONGEI SEC SCHOOL

## KUWA MAKINI NA SUGARMAMY NA FATAKI..!

Kulikuwa na kijana mmoja aitwae Raymond. Raymond alikuwa kijana mwenye akili sana shuleni. Hata hivyo alikuwa anaishi na wazazi wake wote wawili. Wazazi wake walikuwa ni wakulima, hivyo walikuwa na maisha magumusana kiuchumi. Wazazi hawa walijitahidi sana huku na kule ili kijana wao aendelee na masomo yake ya sekondari vema, lakini kadri siku zilivyokuwa zinasonga mbele maisha yao yalizidi kuwa magumu. Kutokana na ugumu wa maisha, ingawa alipenda sana kusoma, Raymond alifukuzwa shule kwa kushindwa kulipa ada kwa miaka miwili aliyosoma kidato cha kwanza na cha pili. Raymond alianza kutafuta vibarua vya hapa na pale ili kujikimu yeye na pia kuwasaidia wazazi wake.

Siku moja Raymond alipokuwa akipita barabarani kutafuta tafuta alikutana na mama mmoja (Sugar mamy) baada ya kujadiliana na mama huyo kwa muda mrefu kidogo, mama huyo alimuahidi kuwa aende akafanye kazi kwake na pia alifurahi sana hasa kwa vile aliambiwa atapelekwa shule.

Raymond alienda kuwaeleza wazazi wake, nao pia walifurahi na wakamruhusu kwenda huko kwa huyo mama. Siku inayofuata Raymond alikwenda kwa yule mama na kuanza kazi nyumbani kama walivyokubalian alifanya kazi kwa bidii sana na yule mama alimpeleka shule ili Raymond asidhani kuwa anadanganywa. Hivyo alifanya kazi za nyumbani na pia aliwea kuendelea na masomo.


Baada ya miezi mitatu yule mama akaanza zake, siunawajua ndugu!! Masugar mamy walivyo!! kumbe yule mama hakuwa na nia ya kumsaidia Raymond lengo lake lilikuwani kumtaka kimapenzi. Siku moja usiku sugar mamy huyo alimuita Raymond chumbani mwake huku akiwa amefunga kanga moja tu nyepesi. Raymond alipokwisha ingia chumbani humo mama huyo alifunga mlango na kuanza kumshinikiza kufanya naye

## .......KUWA MAKINI NA SUGARMAMY NA FATAKI..!

mapenzi. Kwakuwa Raymond hakuwahi kufanya ngono na hata hivyo mama huyo alikuwa mkubwa sawa na mama yake aliogopa na kutetemeka sana hivyo alikataa. Mama huyo alizidi kumshinikiza na kumtishia kumwachisha shule, kazi na kumuua. Hivyo kijana huyo kwa kuzidi kuogopa na kila sababu aliyotoa kukataliwa, alifanya mapenzi na jimama hilo ingawa hakupenda kufanya hivyo kwa kuwa sugar mamy tabia yake si nzuri, hivyo aliendelea na mchezo huo wa kumlazimisha Raymond kufanya naye ngono kila wakati. Kwa kuwa Raymond alikuwa akifanya hivyo bila kupenda na aliona mchezo huo unaendelea na hata yeye kushindwa kwenda shuleni kwa kuwa alijisikia vibaya na aibu sana, mama huyo alianza kumnyanyasa na pia masugar mamy kama kawaida yao alikuwa akiwachukuwa vijana wengine wadogo na kufanya nao ngono kwa nyakati tofauti.

Jimama hilo kwa kuwa lilishaanza kumchoka Raymond, hivyo alizidi kumnyanyasa na pia alimfukuza Raymond kwake na kudai kuwa ni mwizi. Raymond alirudi nyumbani kwa wazazi wake na kuwaeleza yote yaliyompata bila kuficha huku machozi yakimdondoka mithili ya bomba itoayo maji. Wazazi wake walihuzunika sana kwa alichotendewa kijana wao. Baada ya miezi sita afya ya Raymond ilianza kuzorota na kuanza kuugua magonjwa yamara kwa mara ikiwwa ni pamoja na kuharisha, Hivyo kwa kuwa hakuwa na hela ya matibabu, afya yake ilizidi kuzorota na kukonda mno hadi akajitokeza msamaria mwema na kumpeleka hospitali ya mkoa wa Tanga. Raymond alipimwa na daktari aligundua kuwa ameambukizwa virusi vya UKIMWI. Hivyo daktari alimpa ushauri nasaha na kampa matumaini sana na pia alimshauri vyakula vya kula na kufanya mazoezi ili aweze kuendelea kuishi ikiwa ni pamoja na kumpa dawa za kurefusha maisha (ARV). Kwakuwa mipango ya Raymond haikutimia naye alitamani kutimiza ndoto yake na hali ya maisha yao ilikuwa ngumu sana Raymond alikuwa akilia, kuwaza na kujutia kwenda kwa sugar mamy yule bila kujitambua na hata hivyo Raymond alichanga nyikiwa kutokana na mawazo. Miezi mitano baadae Raymond alifariki dunia kwasababu afya yake ilikuwa mbaya mno kwa kushindwa kupata lishe bora kwa ugumu wa maisha. Kabla ya kifo chake alikuwa akilia na kusema kila mara "Ndugu na marafiki zangu jamani nawashauri jiepusheni sana na ngono na kuweni makini na wanao jidai kuwasaidia katika shida zenu, kwani wengi wao ni masugar mamy na mafataki wata waambukiza virusi vya UKIMWI mkafa bure kama ninavyokufa mimi"

**KIGONIGONI SECONDARY SCHOOL , FIGHTING AGAINST AIDS GROUP (FAAG)**




# KISA CHA JOTI:

Joti ni mvulana ambaye anaishi na wazazi wake katika kijiji cha Chanjagaa Wilayani Same mkoani Kilimanjaro. Alikuwa akiishi na wazazi wake wote wawili. Baba yake anaitwa Mboriko na mama yake anaitwa Zeituni na pia alikuwa mtoto wa pekee katika familia yao lakini maisha yao yalikuwa duni sana. Wazazi wake walijitahidi na kufanya kila mbinu ili tu mtoto wao aweze kuhitimu elimu yake ya sekondari.Hatimaye Joti alihitimu elimu ya sekondari katika shule ya sekondari Chanjagaa matokeo yake hayakuwa mazuri, ikawa pigo kwa wazazi wake kwani walitegemea kuwa angefanya vizuri kuwa mkombozi katika maisha yao.

Baada ya matokeo hayo Joti hakuweza kuendelea na chochote kwani alipata sifuri. Joti hakuwa na saada wowote hivyo aliamua kwenda Same mjini kuwa mmachinga. Joti aliifanya kazi hiyo kwa muda wa mwaka mmoja namiezi mitatu bila ya mafanikio yeyote kwani pesa ambayo alipata alitumia kwa ajili ya chakula na mahitaji mengine madogomadogo lakini pia Joti alikuwa tayari kashajiingiza kwenye mapenzi kutokana na kikundi alichokuwa nacho. Baada ya miezi kadhaa Joti alifahamika kila sehemu kutokana na tabia yake kufanya mapenzi na wanawake tofauti. Maisha yake yakawa ni wasichana muda wote`na hela yake nayo ikawa inaishia kwa wasichana. Basi ikafika kipindi Joti anakosa pesa ya chakula lakini pia alikosa pesa ya kuwapa wasichana zake. Hivyo alijikuta amejiingiza katika kufanya ngono na machangudoa (sugar mamy) ili tu waweze kumpatia pesa ambayo itamkidhi katika mahitaji yake. Kwa kuwa alikuwa akihitaji pesa kwajili ya chakula lakini pia kwa ajili ya kuwapa wasichana zake. Joti aliendelea na kitendo hicho kwa muda wa miezi isiyopungua minne. Mwisho wa siku akaacha shughuli yake ya mwanzo na kurudi kijijini.

Joti afya yake ilianza kudhoofika, akawa na dalili zote za virusi vya UKIMWI. Sikumoja aliamua kwenda hospitali ili akapate uhakika kuhusu afya yake kwani tayari Joti alikuwa kashachoshwa na ugonjwa ambao alikuwa akiuhisi kutokana na tabia yake aliyokuwa nayo akiwa Same. Joti alijikokota peke yake mpaka kituo cha afya cha Tumaini kilichopo wilayani Same. Na vipimo vilionyesha kuwa ameathirika kwa UKIMWI. Daktari alimpa ushauri nasaha na akaanza dawa za ARV, Joti akaenda kufanyia kazi ushauri namatumizi sahihi ya daw za kurefusha maisha(ARV) baada ya hapo akapata nafuu na afya yake ikawa nzuri. Hivyo maisha yake yakaendelea kuwa ya kawaida akajihusisha na shughuli za nyumbani kwao. Akajiepusha na wasichana na hakuwa na mpango wa kuoa kabisa kutokana na mateso aliyoyapata. Kwa sasa Joti ameanzisha kikundi chake cha kupambana na maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

**BARAKA NGALITO, KWANGU SEKONDARI**





**Mwl. Cletus Marenge**

Tangu tumepata mafunzo ya mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU toka SMECAO mwaka 2011 mwezi machi,tumeweza kuona manufaa makubwa kwa wanafunzi mashuleni lakini pia kwa jamii inayotuzunguka. Wanafunzi wameelimika na kuweza kubadili na kupunguza mienendo yao mibaya shuleni na hata majumbani.

Hali hii imedhibitishwa na wanafunzi (Wasichana) kwa kukiri kutokuwa na marafiki wa kiume waliokuwa wakishirikiana kimapenzi, pia tabia za wanafunzi kutoka nje ya shule wakati wa mapumziko na kwenda migahawa ya jirani na kupewa ofa za vyakula ikiwa ni moja ya vishawishi vya maambukizi ya vvu zimepungua kwa kiasi kikubwa.

Pia wanafunzi wameelewa na kujiepusha na mazingira hatarishi ya maambukizi ya VVU na baadhi yao wanaeleza kwa ujasiri kwamba hawashiriki kwenye madisco na klabu za usiku, pia hawashawishiki kwa zawadi toka kwa mafataki na masugar mamy.

Pia wanaklabu wamekua chachu kwa jamii pale walipopata nafasi ya kufikisha ujumbe wa ukimwi kwa njia ya nyimbo, ngoma na sanaa ya maigizo. Pamoja na mafanikio hayo bado tunaendelea kutoa elimu kwa kutumia njia shirikishi kwa wanafunzi wachache ambao bado mienendo yao haijarekebika, tunatarajia mafanikio zaidi katika kipindi kijacho.

Tunashukuru shirika la Smecao kwa ushirikiano wao katika vita dhidi ya ukimwi kupitia elimu mashuleni.

**Imeandaliwa na:**
**Mwl. Cletus Marenge**
**Shule ya Vudee Sekondari**

## *KATUNI SHOW*

**na Athuman D. Athuman**



# Same and Mwanga Environmental Conservation Advisory Organization (SMECAO)

**Jarida hili hutolewa na**
**SMECAO FUND,**
**P.O BOX 87,**
**SAME - KILIMANJARO,**
**Email: smecao@gmail.com,**
**smecao@elct.org,**
**Website: www.smecao.jimdo.com**